TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI

MANYONI

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. HW/X.1/1 VOL.III/176** 04 Julai, 2025

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye Sifa kujaza nafasi za kazi zifuatazo;-

**1.0. WATOZA USHURU KATIKA VYANZO MBALIMBALI VYA MAPATO (NAFASI 30)**

**1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA**

- Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Kidato cha Sita (VI) na kuendelea
- Mwenye uzoefu na kazi ya kutoza ushuru na matumizi ya POS na mwenye rekodi ya uadilifu atapewa kipaumbele.

**1.2. KAZI NA MAJUKUMU YA MTOZA USHURU**

i. Kuhakikisha kila anayepaswa kulipia ushuru na tozo za Halmashauri katika chanzo cha kukusanya/kizuizi analipa ushuru stahiki.

ii. Kuhakikisha kuwa fedha zote zilizokusanywa zinawekwa benki sio zaidi ya masaa 24 kutoka zilipokusanywa

iii. Kuhakikisha POS wakati wote zipo salama na zinafanya kazi bila kuwa na matatizo

iv. Kuripoti tatizo lolote la POS kwa Wataalam wa IT kwa ajili ya marekebisho

v. Wakati wote kuwadhibiti wakwepa ushuru hata ikibidi kuripoti ngazi ya Halmashauri kwa hatua zaidi.

vi. Kufanya kazi nyingine utakazopangiwa na Mwajiri/Msimamizi wako

**2.0. ASKARI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI (NAFASI 05)**

Awe amehitimu Darasa la Saba na Kuendelea ambaye anaweza kusoma na kuandika vizuri na awe **amehudhuria na kufaulu mafunzo ya Mgambo** yanayotolewa na jeshi letu la Wananchi na kutunukiwa cheti cha kuhitimu.

i. Kushiriki operesheni mbalimbali za usafi wa mazingira, malipo ya tozo mbalimbali za Halmashauri.
ii. Kuhakikisha usalama kwenye maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ya watu
iii. Kuhakikisha wananchi wanatekeleza sheria mbalimbali za Serikali kuu na Sheria ndogo za Halmashauri
iv. Kudhibiti watoroshaji wa bidhaa mbalimbali zinazopaswa kulipiwa ushuru wa Halmashauri.
v. Kufanya kazi nyingine utakazopangiwa na Mwajiri/Msimamizi wako

**3.0 MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na Mkazi wa Manyoni
ii. Awe na umri usiozidi miaka 45
iii. Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Wasifu) yenye Anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
iv. Waombaji waambatishe nakala za vyeti Kidato cha Nne (Form IV) na Kidato cha Sita (Form VI), Taaluma na Cheti cha Kuzaliwa. Waombaji watakaowasilisha "Result Slip","Statement of Result","Provisional Results", au "Tanscripts" **HAVITAKUBALIKA**.
v. Barua za maombi zilizosainiwa na mwombaji zinaweza kuandikiwa kwa lugha kiingereza na Kiswahili
vi. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **20/07/2025**
vii. Maombi yatayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika Tangazo hili **HAYATAFANYIWA KAZI**.

**Maombi yatumwe** kupitia anuani ya:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni,
S.L.P 60,
**MANYONI.**

**Tangazo hili limetolewa na:**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI

Anastazia Tutuba
MKURUGENZI MTENDAJI (W)